land portal

# Ajenda ya Urekebishaji wa Sera ya Ardhi Nchini Kenya

Ripoti ya webinaa

EUROPEAN UNION

Food and Agriculture Organization of the United Nations

Kenya Land Alliance

REPUBLIC OF KENYA

www.landportal.org

Webinaa kuhusu Urekebishaji wa Sera ya Ardhi Nchini Kenya ilifanyika tarehe 10 Oktoba, 2018. Webinaa ilipitia mchakato wa urekebishaji wa Sera ya Ardhi nchini Kenya na ikashughulikia changamoto anuwai. Lengo lilikuwa kubaini hatua za kufuata zitakazoleta usawa na haki katika urekebishaji wa sera ya ardhi.

Webinaa ilishughulikia maswali yafuatayo:

- Tumefika wapi katika mchakato wa urekebishaji wa Sera ya Ardhi?
- Changamoto kuu zinazohitaji kushughulikiwa katika mfumo wa urekebishaji wa Sera ya Ardhi na matumizi ya ardhi ni zipi?
- Umuhimu wa jinsia katika urekebishaji wa Sera ya Ardhi unaweza kufanikishwa kwa namna gani?
- Athari za kuuza ardhi ya jamii ni zipi?
- Uhifadhi wa data kidijitali unashughulikia kwa namna ukinzani uliopo katika ofisi zinazohusika na rekodi za ardhi?

**Webinaa iliandaliwa kwa ushirikiano wa Kenya Land Alliance (KLA), Serikali ya Kenya, Wakfu wa Tovuti ya Ardhi, Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa, na Muungano wa Uropa.**

**Msimamizi:** Michael Ochieng Odhiambo, Director of People, Land and Rural Development (PLRD)

**Wanajopo:**

- Dkt. Collins Odote Oloo, Mhadhiri Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Nairobi
- Odenda Lumumba, Afisa Mkuu, Shirika la Masuala ya Ardhi Nchini Kenya (KLA).
- Husna Mbarak, Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO)

Watu 132 walijisajili kwa webinaa na hatimaye watu 58 walishiriki.

**Video kamili ya webinaa hiyo inapatikana katika YouTube:**
**https://youtu.be/IDGEpHrK95U**

## Masuala makuu yaliyojitokeza

- Kuna sera na sheria imara kuhusu urekebishaji wa Sera ya Ardhi nchini Kenya, hata hivyo hakuna maendeleo mengi ambayo yamepatikana katika kufanikisha matarajio ya mchakato wa urekebishaji wa sera ya ardhi katika utendaji.
- Mifumo ya utekelezaji bado ingali goigoi
- Ikija kwa mihimili ya urekebishaji wa Sera ya Ardhi nchini, ushirikiano miongoni na pia baina ya asasi kuu ni muhimu. Lengo linapasa kuwa kuendelea kuvipa nguvu vikundi vya kiraia, sekta ya kibinafsi na vikundi vya kijamii ili vifanye kazi kwa ushirikiano.
- Kuhusu umuhimu wa jinsia katika urekebishaji wa Sera ya Ardhi, tumeona kuwa idadi kubwa ya wanawake inapata ardhi, lakini kuna haja ya utekelezaji wa kiasi kilichowekwa kikatiba kitakachoendeleza usawa na usawazisho
- Kwa upande wa haki ya ardhi ya jamii nchini, mojawapo ya changamoto itakuwa kufuata masharti yaliyopo.
- Nchi na wizara inajaribu mchakato wa kuhifadhi rekodi kidijitali. Tayari njia hii inaonekana imara ya kuweka rekodi na pia kuhakikisha utendaji bora wa kazi. Tatizo kubwa zaidi ni kuthibitisha kwamba kuhifadhi rekodi hizi kidijitali kutahakikisha usalama.

## Mukhtasari wa Webinaa

### 1) TUKO WAPI KATIKA MCHAKATO WA UREKEBISHAJI WA SERA YA ARDHI NCHINI KENYA?

- Mchakato wa urekebishaji kutoka upande wa utungaji sera **umekwama** katika kiwango cha utekelezaji. Mihimili ya sera, utungaji sheria na asasi tayari imewekwa, lakini **hatua za utekelezaji ni goigoi**.
- Wadau wanatafuta jinsi watafanya utekelezaji wa urekebishaji wa Sera ya Ardhi ufanyike, jambo ambalo limekuwa **tatizo kubwa**.
- **Kenya ina sera na sheria "nzuri"**, hata hivyo, hakuna maendeleo mengi yanayopatikana katika kufanikisha ndoto ya urekebishaji wa Sera ya Ardhi.

### 2) CHANGAMOTO KUU ZINAZOHITAJI KUSHUGHULIKIWA KATIKA MIHIMILI YA UREKEBISHAJI WA SERA YA ARDHI NI ZIPI?

- Siku hizi, mtu anaweza kuhesabu idadi ya mashirika yanayoshughulikia masuala ya ardhi. Inatakikana juhudi zilenge zaidi kuwezesha **vikundi vya kiraia**, sekta ya

kibinafsi, na vikundi vya kimaendeleo vya jamii kufanya kazi pamoja.

- Changamoto kuu ni pamoja na mashirika na asasi zisizo na uwiano ambazo zimepewa kazi ya kusimamia ardhi na maliasili.
- Asasi mpya zinajengwa. Changamoto kuu ni **ukosefu wa ushirikiano miongoni mwa asasi.**
- **Bajeti ya tume mbalimbali inaendelea kuwa finyu.** Hakuna mantiki yoyote katika kufikiria kuhusu urekebishaji wa sera ya ardhi bila kukadiriwa bajeti.

### 3) UMUHIMU WA JINSIA KATIKA UREKEBISHAJI WA SERA YA ARDHI UNAWEZA KUTEKELEZWA VIPI?

- Kanuni zinazounga mkono **vitendo vya kuleta usawa wa kijinsia** katika upande wa ardhi na rasilimali lazima zitekelezwe. Kwa mfano, tumeona msisitizo katika programu za kutoa vyeti miliki, lakini tukiangazia wanawake, tunaona kuwa bado tuko mbali kuwawezesha ili kubadilisha hali yao ya kiuchumi.
- Idadi ya wanawake wanaopata ardhi imeongezeka, l**akini kiasi kilichowekwa kikatiba kinachokuza usawa na usawazisho wa kijinsia** ni lazima kitekelezwe.
- **Dhima ya wanawake** na umuhimu wa ufanikishaji **zimedunishwa kwa kupendelea wanaume.**

### 4) ATHARI ZA UUZAJI WA ARDHI YA JAMII NI ZIPI?

- Matokeo ya kutambulikana, kulindwa na kusajiliwa kwa ardhi ya jamii kama mali ya jamii yanapata pingamizi kutokana na kuwa ardhi ya jamii ndiyo hulengwa na miradi mikubwa katika Dira ya 2030. Sheria za kutoa kufidia kote Afrika Mashariki zinapitiwa tena ili kukwepa sera mpya kuhusu uuzaji wa ardhi ya jamii.
- Mojawapo ya changamoto bado ingali **nia ya kisiasa** katika kufuata sheria za haki za ardhi ya jamii.

### 5) UHIFADHI WA DATA KIDIJITALI UNASHUGHULIKIA UKINZANO ULIOPO KATIKA OFISI ZINAZOHUSIKA NA REKODI ZA ARDHI KWA NAMNA GANI?

- Nchi na wizara zinajaribu kuweka rekodi ya ardhi kwenye mchakato wa kidijitali. Njia hii imeonekana kuwa salama katika kuhifadhi rekodi; pia itahakikisha utendaji bora wa kazi, na pia kupunguza mzigo wa kufanya mambo kwa mikono. Kuingiza data kwenye mfumo wa dijitali ni njia nzuri ya kuondoa ufisadi na kuboresha utenda kazi.
- Tatizo kubwa zaidi ni kuhakikisha kwamba uhifadhi huu wa data kidijitali utahakikisha usalama.
- Zaidi ya hayo, ilhali kuna tegemeo la mazuri kuhusu uhifadhi data kidijitali, ni lazima tuhakikishe juhudi za uhifadhi huu hazifanyiki tu kwa minajili ya kukusanya kodi. Hasa, wakati vipande vikubwa vya ardhi chini ya umiliki wa jamii havijasajiliwa.

## Baadhi ya Kauli kutoka kwa wanajopo



"KUZINDULIWA KWA SERA YA KITAIFA YA ARDHI NA KATIBA YA KENYA YA 2010 KULIKUWA MAFANIKO YA KIPEKEE KATIKA UREKEBISHAJI WA SERA YA ARDHI, LAKINI MIAKA MINANE BAADAYE, BADO KUNA CHANGAMOTO YA TOFAUTI ZA KIJINSIA, KUTOKUWA SALAMA KWA SERA YA ARDHI YA JAMII NA USIMAMIZI MBAYA WA ARDHI ".

-MICHAEL OCHIENG ODHIAMBO, MKURUGENZI WA "PEOPLE, LAND AND RURAL DEVELOPMENT" (PLRD)



"TUNA SERA NZURI, LAKINI TUNA MIFUMO ILIYOWEKWA AMBAYO HUKINZANA YENYEWE KWA YENYEWE. USIMAMIZI WA ARDHI KATIKA NCHI HII UMESHINDWA KUDHIBITI MFUMO HUU WOTE. TUNAHITAJI KUPIGANIA UREKEBISHAJI WA ASASI."

- HUSNA MBARAK, SHIRIKA LA CHAKULA NA KILIMO LA UMOJA WA MATAIFA (FAO)



"CHANGAMOTO KUU NI MASHIRIKA YASIYOUNGANA NA ASASI ZILIZOPEWA DHIMA YA KUSIMAMIA ARDHI NA SEKTA YA MALIASILI; NA ZAIDI KUSHINDWA KWA TUME YA KITAIFA YA ARDHI KUTEKELEZA WAJIBU WAKE WA KURATIBU, KUFUATILIA NA KUSIMAMIA ARDHI."

- ODENDA LUMUMBA, CEO, KENYA LAND ALLIANCE



"UHIFADHI WA DATA KIDIJITALI NI MBINU BORA KABISA KWA SABABU ITASAIDIA KUONDOA UFISADI NA KUBORESHA UTENDAKAZI. KADRI UREKEBISHAJI WA SERA YA ARDHI UNAVYOENDELEA NA KUKAMILIKA KUINGIZWA KWENYE MFUMO WA KIDIJITALI SHARTI TUELEWE KUWA, KWA BAHATI MBAYA, FIKRA ZETU KAMA NCHI ZIKO KATIKA UTENDA KAZI KWA MIKONO."

- DKT. COLLINS ODOTE OLOO, MHADHIRI MWANDAMIZI, CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

**LAND PORTAL FOUNDATION**
Postbus 716, 9700 AS Groningen, the Netherlands
www.landportal.org | hello@landportal.org